# Mustakabali wa Tungo za Ngonjera katika Fasihi ya Kiswahili

Esther J. Masele

**Ikisiri**

Ngonjera katika kipindi cha kabla na baada ya ukoloni zilionekana kuwa ni njia bora na rahisi ya uelimishaji wa mambo muhimu ya kisiasa na kijamii. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1990 ngonjera zimeonekana kupoteza kabisa umaarufu wake. Lengo la makala hii ni kujadili chimbuko la ngonjera, umuhimu wake kwa jamii na mambo mbalimbali yaliyosababisha ngonjera kupoteza umaarufu wake. Makala hii ni sehemu ya utafiti uliofanywa na mwandishi kwa wanafunzi walimu wanaosomea shahada ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania ambapo data zilipatikana kwa kutumia njia mbili: udurusu wa nyaraka hasa zile zilizojadili kuhusu ngonjera pamoja na usaili. Utafiti huu ulitumia sampuli lengwa ili kuteua wasailiwa na nyaraka za kudurusiwa. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa matumizi ya ngonjera yameshuka au inaweza kusemwa kuwa hayapo katika ulingo wa fasihi tofauti na aina nyingine za ushairi. Miongoni mwa sababu zilizotajwa kuchangia anguko hilo ni dhana ya kuwa ngonjera ni zana iliyotumika kueneza sera za siasa ya ujamaa na kujitegemea. Dhana hii imechangia kukosekana kwa soko la ngonjera katika kipindi hiki kilichotawaliwa na siasa za vyama vingi, jambo lililowafanya waandishi kutojikita katika utunzi wa ngonjera. Mwitikio huu hafifu umesababishwa na kukosekana kwa msisitizo wa elimu kutoka katika ngazi mbalimbali za elimu pamoja na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa ngonjera. Mwisho makala imeshauri njia mbalimbali zinazoweza kuhuisha matumizi ya ngonjera ikiwa ni pamoja na kuingiza ngonjera katika mitaala ya elimu ili ziweze kutumika kama njia ya kufundishia mada zinazohitaji mdahalo. Makala hii imejifungamanisha zaidi kwa mtunzi maarufu wa ngonjera, hayati Mathias Eugen Mnyampala katika mifano na majadiliano.

## 1.0 Utangulizi

Ngonjera ni aina ya ushairi ambao ulishamiri sana hapa Tanzania hasa katika kipindi cha miaka ya 1970 hadi 1980. Hiki kilikuwa ni kipindi ambacho Tanzania ilikuwa katika hali ya kujijenga upya baada ya kutoka mikononi mwa utawala wa kikoloni. Aina hii ya tungo ilionekana kuwa na mvuto mkubwa kwa Watanzania hasa kwa vile ilionesha mafanikio makubwa katika kuielimisha jamii juu ya mambo mbalimbali yahusuyo nchi yao. Vilevile, kuibuka kwa ngonjera kuliongeza utajiri mkubwa katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, kadiri siku zilivyokuwa

zikienda ngonjera zilizidi kupotea katika matumizi yake ya kawaida. Hivyo, lengo la makala hii ni kujadili mustakabali wa tungo hizi katika fasihi ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hili makala inachunguza sababu za ngonjera kupoteza umaarufu wake nchini Tanzania. Aidha, makala inatathmini umuhimu wa ngonjera katika jamii pamoja na kupendekeza njia mbalimbali zinazoweza kusaidia kuziboresha ili ziweze kurudi katika matumizi yake kama ilivyokuwa hapo awali.

Makala hii ni zao la utafiti uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma nchini Tanzania. Utafiti ulitumia usampulishaji lengwa ili kuteua wasailiwa na nyaraka za kudurusiwa. Udurusu wa maandishi ulitumika kwa kiasi kikubwa ambapo diwani za Mnyampala pamoja na maandiko mengine yaliyomzungumzia mshairi huyu yalisomwa na kuchambuliwa kulingana na lengo la utafiti. Usaili ulitumika kwa kiasi kidogo na ulilenga zaidi kupata maoni ambayo yangesaidia zaidi katika ufafanuzi na kupata mtazamo wa jamii juu ya mada tafitiwa. Usaili huu ulifanywa kwa wanafunzi walimu waliokuwa wakisomea shahada ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili ambapo "Ushairi wa Mshairi Teule" ambaye ni Mathias Mnyampala ilikuwa mojawapo ya kozi waliyoisoma.

Ili kufanikisha makala hii, kazi hii imegawanywa katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi na usuli wa ngonjera, sehemu ya pili inajadili umuhimu na malengo ya ngonjera, sehemu ya tatu inajadili mambo yaliyosababisha ngonjera kupoteza umaarufu wake, na sehemu ya nne inatoa mapendekezo na hitimisho.

## 2.0 Usuli wa Ngonjera

Sehemu hii inatoa mwongozo wa mambo mbalimbali yanayohusiana na mada lengwa ikiwa ni pamoja na ufafanuzi wa dhana ya ngonjera na historia yake kwa ufupi.

### 2.1 Dhana ya Ngonjera

Ngonjera ni neno lenye asili ya Kigogo ambalo maana yake ni 'twende pamoja.' Istilahi hii hutumika kurejelea hali ya watu kwenda sambamba katika mazungumzo yao (Mulokozi na Sengo, 1995). Ngonjera ni utanzu wa ushairi unaotumia malumbano na mahojiano kati ya watu wawili au zaidi ambao huwa na muundo wa mashairi ya kimapokeo (Massamba, 1983; Ndulute, 1985; Mgute, 2012). Katika aina hii ya ushairi, kama inavyoelezwa na Njogu na Chimerah (2008), mhusika mmoja huwa anajua mambo zaidi ya kile kinachozungumziwa kuliko mhusika au wahusika wengine. Vilevile, Mgute (2012) anafafanua kuwa majibizano haya hulenga kutoa jibu au suluhisho kuhusu tatizo au jambo linalojadiliwa katika ngonjera hizo. Akirejelea *Ngonjera za UKUTA*[1], Masungwa (2012) anaeleza kuwa

[1] Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania.

ngonjera hutumia lugha rahisi na inayoeleweka kwa watu wote. Lugha hii huwa ni ya mkato na yenye maneno teule. Kwa kawaida, jibu au suluhisho la mada inayojadiliwa hupatikana mwishoni mwa ngonjera. Vilevile, Mnyampala (1970) anaeleza kuwa ngonjera ni ushairi rasmi ambao ulilenga kulihami taifa na athari za kikoloni, yaani kuondoa mawazo yaliyosadikishwa kwa watu kuwa kila kitu cha Kiafrika ni cha kishenzi. Kwa ujumla, ngonjera ni aina ya ushairi wa majibizano ambao huwa na pande mbili, yaani upande wa anayehitaji kufahamishwa na upande wa mfahamishaji. Lengo hasa la majibizano hayo ni kutaka kuielimisha jamii juu ya mada husika.

## 2.2 Historia ya Ngonjera

Istilahi hii ya ngonjera, kama inavyoelezwa na Harries (1962), inarejelea mashairi ya kujibizana ambayo yalikuwapo tangu enzi za Muyaka bin Haji (1776-1840)[2] kuanzia miaka ya 1800. Akibainisha jambo hili Chiraghdin (1973) kama alivyonukuliwa na Massamba (2003:76) anasema kuwa mtindo huu ulikuwapo hasa sehemu za Mvita huko Kenya na ulikuwa ukiitwa 'kufunga nyama', yaani malenga wawili walikuwa hawaonani wakati wakiwa katika malumbano yao. Wakiwa katika utendi huu mara zote walitengwa na pazia na kuzungukwa na watu. Katika majibizano hayo malenga mmoja aliuliza maswali na wa pili alijibu mashauri. Zoezi hili liliendelea mpaka mjibu maswali afungue 'nyama', yaani alifumbue fumbo hilo. Ni vigumu kuitaja tarehe ya kuanza kwa ushairi wa majibizano, lakini tunaweza kusema ushairi wa aina hii ni mkongwe sana, kwani ulianza tangu enzi ambazo ushairi ulikuwa ni nyimbo tu zisizozingatia arudhi. Manju mmoja katika kikundi cha watu alitongoa wimbo wake wote kisha akakaa chini. Ndipo manju mwingine pia kutoka katika kikundi kingine alisimama na kutongoa wa kwake ikiwa ni jawabu la wimbo wa malenga wa kwanza. Ngonjera za namna hii zilishamiri sana katika sehemu ya Pemba (Massamba, 1983). Katika kuelezea historia ya ushairi wa majibizano, Chiraghdin (1974) anasema kuwa huko Kaskazini mwa Lamu majibizano ya namna hii yalisimamiwa na shaha wa malenga, yaani mkuu wa manju. Ilipotokea kwamba mmoja ameshindwa basi yule shaha alimvika 'guni', yaani alimtia hila kwa kushindwa kwake katika utangazaji wa mashairi.

Historia ya kuwapo kwa ngonjera katika jinibu za Waswahili wa bara ilinasibishwa na Bwana Mathias Eugen Mnyampala[3]; mmoja wa washairi bingwa si tu katika Tanzania bali pia Afrika Mashariki. Licha ya kuandika mashairi, Mathias Mnyampala alikuwa ni miongoni mwa watu waliotoa mchango mkubwa

---

[2] Mshairi maarufu kutoka nchini Kenya.

[3] Mshairi na mwanasiasa maarufu nchini Tanzania ambaye alizaliwa mwaka 1917 na kufariki mwaka 1969. Pia, aliwahi kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa taifa ikiwa ni pamoja na ualimu na ukarani katika ofisi mbalimbali.

katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni nchini Tanzania. Harakati zake za kuandika ngonjera zilianza rasmi pale alipojiunga na vyama vya TAA (Tanganyika African Association) na hatimaye TANU (Tanganyika African National Union). Hivyo, alitumia nafasi yake ya kisanii kueneza sera za vyama hivi, jambo lililozifanya ngonjera kufahamika kwa haraka nchi nzima. Kupitia ngonjera, Mathias Mnyampala alijitahidi kuuelimisha umma wa Watanzania juu ya TANU na sera zake. Alisisitiza kuwa wakulima na wafanyakazi ndio wangekuwa wa kwanza kufaidika na chama hicho. Njia hii iliwahamasisha watu wengi kujiunga na chama cha TANU. Alitumia ngonjera kuwaelimisha kuwa chama cha TANU pekee ndicho kilichokuwa na uwezo wa kuwaunganisha watu wa dini na makabila yote. Watu wengi waliweza kuelewa kwa urahisi madhumuni ya chama cha TANU ambayo yalikuwa na lengo la kudumisha uhuru, kulinda heshima ya taifa pamoja na kudumisha demokrasia ya kweli. Mnyampala alikuwa na imani kubwa na chama cha TANU na alikuwa na uwezo mkubwa wa kuhamasisha watu. Pia alishuhudia jinsi ngonjera zilivyozaa matunda katika kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, kwake ngonjera zilikuwa ni ukombozi kwa Watanzania. Akifafanua juu ya umuhimu huo anasema:

> Watu wengi waliosoma vizuri Kiingereza wanafahamu sifa za mashairi na michezo mingi ya mshairi mashuhuri Shakespeare wa Uingereza. Kwa bahati njema, taifa letu nalo limevumbua njia za ushairi na michezo inayofanana na hiyo ya Shakespeare, lakini yenye mazingira ya Watanzania wenyewe, yaani lugha ya Kiswahili, utamaduni wa Watanzania na shabaha maalumu ya Kitanzania (Mnyampala, 1971:1).

Mnyampala aliona kuwa ngonjera zinabeba jukumu kubwa kama ilivyokuwa kwa mashairi ya Shakespeare. Aliamini kuwa kupitia ngonjera Watanzania wangeweza kujifunza mambo mengi kwa wepesi zaidi kwani kilichohitajika ni uwezo tu wa kukariri.

Pia, ifahamike kwamba, Mathias Mnyampala ndiye aliyebatiza ushairi huu kwa jina la ngonjera katika diwani zake za *Ngonjera za UKUTA* (namba moja na mbili) alizozichapisha katika miaka ya 1970 na 1971 kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

> Kazileta Mnyampala, wa UKUTA kazichora
> Ya siasa na muwala, ya busara na ubora
> Hayana ndani shakala, ila ya njema fikira
> Maana yake Ngonjera, ni mafunzo kwa shairi.
> (Mnyampala, 1970: 6).

Mnyampala alizipa diwani zake jina la *Ngonjera za UKUTA* kutokana na ukweli kwamba yeye ndiye alikuwa kiongozi wa chama cha UKUTA na si mwanzilishi wa mashairi ya majibizano au malumbano kama ilivyoandikwa na baadhi ya wataalamu wa lugha. Hata hivyo, dhana hii potofu ya kuwa ngonjera zilianzishwa na Mathias Mnyampala ilionekana kutawala katika vichwa vya watu jambo lililowafanya baadhi ya wataalamu kuweka ufafanuzi juu ya jambo hili. Kwa

mfano, Massamba (2003: 76) anasema, “watu wengine wamekuwa wakidhani kwamba ngonjera zilianzishwa na Mathias Mnyampala, hasa kwa kuwa yeye aliwahi kuandika *Ngonjera za UKUTA*, la hasha, yeye alizihuisha tu.” Katika kufafanua jambo hili Makaka (2012: 16) anasema:

> Ninapenda ieleweke kwamba madai ya Mnyampala na wenzake katika UKUTA si ya kweli hata kidogo. Utanzu huu wa Ngonjera ulikuwapo tangu zamani. Ukweli uliopo ni kwamba Mnyampala na chama cha UKUTA waliihuisha tu na katu hawakuanzisha.

Mawazo ya Massamba na Makaka kuhusu Mathias Mnyampala kuanzisha au kutokuanzisha ngonjera yanaonekana kushabihiana na hivyo kuthibitisha ukweli wa kile kinacholeta utata. Hata hivyo, pamoja na kuondoa utata wa jambo hili wataalamu hawa wanakiri kuwa Mathias Mnyampala ndiye aliyekuwa wa kwanza kwa hapa Tanzania kuweka aina hizi za tungo katika matumizi na kuzifanya kupendwa sana hasa katika shughuli za kisiasa.

## 3.0 Umuhimu na Malengo ya Ngonjera

Pamoja na kuchelewa kuingia katika fasihi ya Kiswahili, ngonjera zilionesha mafanikio makubwa katika kuelimisha jamii. Miongoni mwa faida zilizobainika katika usaili ni pamoja na kutoa elimu ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania, kufunza maadili, kueneza utamaduni, kukuza lugha ya Kiswahili, kukuza vipawa vya kujieleza, kusherehesha sikukuu mbalimbali na kujenga uzalendo kama inavyoelezwa zaidi hapa chini.

### 3.1 Kuelimisha

Ngonjera, kwa kiasi kikubwa, zinaweza kuelezwa kuwa ni njia rahisi ya kufundishia mambo mbalimbali ya kijamii kwani humwezesha mwanafunzi kujua mambo yanayoelezwa pasipo kutumia nguvu nyingi za kusoma. Katika kuthibitisha hili, Mnyampala (1970: 3) anasema kuwa ngonjera ni lazima ziwe na mafunzo ndani yake na kama hazina mafundisho yoyote basi haziwezi kuitwa ngonjera. Ngonjera zinawafunza vijana utamaduni wa taifa lao na mazingira ya nchi yao kwa ujumla. Vilevile, huwafanya vijana hawa kuwa jasiri na wenye kupenda mno taifa lao kuliko mambo mengineyo ya binafsi kama vile ukabaila, ubepari, ubwanyenye, na kadhalika. Mnyampala anaongeza kuwa, kupitia ngonjera, watu walitambua vizuri malengo ya nchi yao kupitia siasa ya TANU, Azimio la Arusha, elimu ya utamaduni, sikukuu za taifa na mahusiano. Mbali na siasa, ngonjera zinaweza kutumiwa kufundishia mambo mengine yanayoikabili jamii ikiwamo ugonjwa wa UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini), athari za utandawazi, dawa za kulevya na mengine yanayofanana na hayo ambayo bado ni changamoto kubwa kwa jamii yetu.

### 3.2 Kuburudisha

Ngonjera ni aina ya mchezo unaokusudia kuwachekesha wasikilizaji na kuwafundisha sawia, hasa zikichezwa jukwaani. Mara nyingi ngonjera zina lengo la kuburudisha na kuwafanya watu wafurahi. Kwa mfano, hivi karibuni kuanzia miaka ya 2000 hapa nchini Tanzania kumekuwapo na kipindi cha FATAKI kinachooneshwa na TBC1 ambacho kina muundo huohuo na kimekuwa kikitumika kuburudisha jamii na wakati huohuo kikitoa mafunzo mbalimbali.

Katika kipindi cha miaka ya 1980 kurudi nyuma wanafunzi wa shule na vyuo walitumia ngonjera ili kunogesha sikukuu, mahafali na sherehe zinginezo. Ngonjera hizo zilikuwa burudani kubwa kwa wasikilizaji wakiwamo wanafunzi na wageni waalikwa. Licha ya kutendwa mashuleni, ngonjera zilitumika sana katika sherehe za kitaifa. Mfano unaonekana katika shairi la "Sikukuu ya Jamhuri" ubeti wa kwanza na wa pili kama linavyosomeka hapa chini:

**Hojaji**

Ipi sikukuu kubwa, na yenye jaha na heri?
Tuipikie ubwabwa, kwa sarara na kidari?
Na au mtukufu kubebwa, kwa mapana na fahari?
Ipi siku mashuhuri, nchini mwetu Tanzania?

**Mwanasiasa**

Ipo sikukuu kubwa, ni hii ya Jamhuri,
Furaha kubwa kwa ubwabwa, hii ni siku ya heri
Ndipo pango lilizibwa, nchi kupata uhuru
Hii siku mashuhuri, uhuru wetu kujipatia.
Mnyampala (1970:65-66).

Katika ngonjera hii kuna wahusika wawili mmoja akihoji swali "Ipi sikukuu kubwa" na mwingine akitoa jibu kuwa sikukuu iliyo kubwa ni Jamhuri kwani inatukumbusha siku tuliyopata uhuru. Kimsingi, sikukuu ya Jamhuri inawakumbusha wananchi siku ambayo Tanzania (bara) ilivua joho la utumwa kutoka kwa Mwingereza mnamo tarehe 9 Desemba, 1961. Ngonjera zingine katika diwani hii ya *Ngonjera za UKUTA I* ambazo zina mwega huu ni zile zinazozungumzia Sikukuu ya Muungano tarehe 26 Aprili ambayo wananchi wa Tanzania husherehekea muungano wa nchi mbili (Tanganyika na Zanzibar) na Sikukuu ya Saba Saba[4].

[4] Sikukuu ya wakulima nchini Tanzania ilikuwa ikiadhimishwa tarehe 7 Julai (Saba Saba) ya kila mwaka. Sikukuu hii mwanzo ilikuwa ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa chama cha TANU kilichozaliwa tarehe 7 Julai 1954. Hata hivyo, kwa sasa sikukuu ya wakulima inaadhimishwa tarehe 8 Agosti kila mwaka na inajulikana kwa jina la Nane Nane.

### 3.3 Kujenga Uzalendo

Mbali na kuburudisha, ngonjera zinasaidia sana katika kukuza uzalendo kwa wasomaji na wasikilizaji. Kwa mfano, *Ngonjera za UKUTA* I & II zinazungumzia masuala mbalimbali ya kizalendo ambayo yalikuwa yakitiliwa mkazo sana na chama cha TANU[5] na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ngonjera hizi zilighanwa na wanafunzi wa ngazi mbalimbali za elimu hasa katika shule za msingi. Kupitia ngonjera hizo wanafunzi walijifunza mambo mengi ya kitaifa ukiwamo umuhimu wa ujamaa vijijini, mwito wa kujitegemea na mwenge wa uhuru. Kwa kuzingatia umuhimu huo, bado tunaweza kusema kuwa ngonjera zinahitajika kufundishwa shuleni kwa wanafunzi wetu ili kuwafunza mambo muhimu ya kitaifa na kiutamaduni.

### 3.4 Kukuza Lugha ya Kiswahili

Licha ya kujenga uzalendo, ngonjera zimeonekana kuwa njia nzuri ya kukuza lugha ya Kiswahili inayozungumzwa katika bara la Afrika, hasa Afrika Mashariki. Hii inatokana na ukweli kwamba, ngonjera ni kipera cha ushairi ambacho hutumia lugha ya kisanii na kuwafanya watu wawe mahiri katika kutumia lugha yao.

Katika utangulizi wa *Ngonjera za UKUTA I*, Rashid Kawawa (aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Tanzania katika serikali ya awamu ya kwanza) alisema kuwa ngonjera zimethibitika kuwajenga vijana kuwa makatibu bora kwa siku za baadaye, jambo ambalo ni la muhimu sana kwa jamii yetu. Pia kwa kuzingatia uwezo mkubwa wanaopata vijana katika kujieleza, ngonjera huwajengea ujasiri hasa wa kusimama jukwaani na kujieleza vizuri na kwa Kiswahili fasaha pasipo mashaka wala woga (Mnyampala, 1970: 1-2).

Kutokana na umuhimu wa ngonjera kwa jamii na hasa ukizingatia malengo yake kama yalivyoainishwa na Mathias Mnyampala na wataalamu wengine, ni ukweli usiopingika kwamba ngonjera ni tungo ambazo zilifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwafanya Watanzania kujua kikamilifu malengo ya nchi yao. Vilevile, kupitia ngonjera watu walijifunza mambo mengi muhimu kwa taifa lao na maisha yao kwa ujumla. Hata hivyo, haikuwahi kuthibitika mambo ya msingi yaliyosababisha aina hii ya ushairi kupoteza umaarufu wake katika ulingo wa fasihi, kwani hata maandiko yanayozungumzia kuhusu ngonjera hayakuwahi kueleza kinagaubaga juu ya jambo hili. Kutokana na sababu hizi andiko hili limejikita katika kuchunguza sababu za msingi zilizofanya ngonjera kupoteza umaarufu wake kama zinavyowasilishwa hapa chini.

[5] Chama kilicholeta ukombozi nchini Tanzania.

## 4.0 Mambo Yaliyosababisha Ngonjera Kupoteza Umaarufu

Kama tulivyosema hapo awali, ngonjera zilikuwa maarufu sana katika kipindi cha kabla ya miaka ya 1980. Umaarufu huu ulianza kufifia taratibu kuanzia miaka ya 1990 hatimaye kupotea katika matumizi ya kawaida. Yapo maswali mengi ambayo mtu anaweza kujiuliza kuhusu jambo hili. Hata hivyo, majibu ya maswali haya hayako wazi sana. Kwa kupitia uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa makala hii, imeweza kubainika kwamba zipo sababu ambazo ni za msingi zilizochangia kufanya ngonjera kupoteza umaarufu wake. Miongoni mwa sababu ambazo makala hii imezibaini ni kama zifuatazo:

### 4.1 Kujifungamanisha zaidi na Kueneza Siasa

Japokuwa ngonjera zimekuwapo kwa muda mrefu, watu wengi nchini Tanzania walikuwa hawajui ngonjera ni nini. Wengi walianza kuzisikia kutoka kwa Mathias Mnyampala, kwa kusoma diwani zake za *Ngonjera za UKUTA* (I & II) (Massamba, 2003:78). Ngonjera hizo zilikuwa zimejikita katika kueneza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea pamoja na sera zingine za chama cha TANU kama inavyodhihirika katika *Ngonjera za UKUTA II*. Pia, suala hili linadhihirika pale ambapo Mnyampala katika dibaji yake ameandika kuwa ngonjera huwafunza wasikilizaji wake mambo mbalimbali yanayohusiana na siasa ya nchi yetu (Mnyampala, 1970: 3). Sababu hii iliwafanya watu wengi kupotoka na kuona kuwa ngonjera ni tungo za ushairi ambazo dhamira yake kuu ni kueneza sera za kisiasa tu.

Kama inavyofahamika siasa ya ujamaa na kujitegemea ilififia na kutokomea baada ya Azimio la Zanzibar mwaka 1990. Hii ni kufuatia kuanguka kwa Jumuiya ya Kisoshalisti ya Watu wa Urusi (USSR) na kushika hatamu kwa sera za kiuchumi za kibepari (Mgute, 2012). Kupitwa na wakati kwa sera hizi kunakotokana na mambo mbalimbali kama vile kuingia kwa vyama vingi na uchumi wa kibepari kumesababisha tungo za ngonjera kuanza kufifia na hatimaye kupotea kabisa. Jambo hili limedhihirishwa na wataalamu mbalimbali wa lugha wakiwamo Ndulute (1985), Mulokozi na Sengo (1995) na Massamba (2003) ambao wanaeleza kuwa *Ngonjera za UKUTA* zilijifungamanisha zaidi na masuala ya siasa, hususan siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo ilikuwa na lengo la kuhakikisha njia zote za uchumi zinamilikiwa na umma. Kwa upande wake, Ndulute (1985:156) anasema kuwa ngonjera za UKUTA zilishindwa kudumu katika ushairi wa Kiswahili kutokana na ukweli kwamba Mnyampala alichagua kuwa “kipaza sauti cha wanasiasa” badala ya kuangalia ukweli kuhusu jamii inayomzunguka. Ndulute anaongeza kwamba hali hii pengine ilisababishwa na wito alioupata kutoka kwa hayati mwalimu Julius Kambarage Nyerere mnamo tarehe 5 Juni 1968 uliomtaka yeye na wasanii wengine kutumia ushairi wa Kiswahili na vipaji vyao kueneza sera za nchi. Hivyo, kupitia ngonjera, Mathias

Mnyampala aliamua kuwafahamisha Watanzania kuwa iwapo watafanya kazi kwa bidii na maarifa wataondokana na kutegemea mikopo kutoka nje, jambo aliloona ni hatari kwa mataifa machanga. Hata hivyo, kuanguka kwa Azimio la Arusha[6] ambalo lilibeba dhana ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kulisababisha ngonjera hizo kupoteza umaarufu wake. Akieleza kuhusu hali ya ngonjera Massamba (2003: 77) anasema:

> Hali ya Ngonjera katika Tanzania, na tuseme siku hizi, inasikitisha sana. Nionavyo mimi, hadhi yake haina utukufu mkubwa kama ilivyokuwa hapo awali. Na hakika siku hizi ukitaja neno 'ngonjera' basi watu wanalinasibisha na masuala ya siasa. Sisemi kwamba ngonjera zisitumike katika kuzungumzia masuala ya siasa la! Ninachojaribu kuonesha hapa ni ile hatari itokanayo na kuzitazama ngonjera kama vyombo vya kisiasa pekee.

Maelezo haya yanathibitisha namna ngonjera zilivyokuwa zimefungamanishwa mno na masuala ya kisiasa jambo lililosababisha watu kuona kuwa ni chombo cha kisiasa. Hivyo, kuachwa kwa mfumo wa chama kimoja mwaka 1992 kulisababisha ngonjera kupoteza umaarufu wake. Hata hivyo, katika *Ngonjera za UKUTA I* zilikuwapo pia ngonjera zenye dhamira zingine tofauti kama vile fitina kazini, wizi wa mifugo, maisha ya nyumba za kupanga na mapenzi na ndoa ambazo Ndulute (1985) anaeleza kuwa zilikuwa katika muegamo wa mfumo dume.

## 4.2 Mwitikio Hafifu wa Wasomi katika Utunzi na Uandishi wa Ngonjera

Mbali na kujifungamanisha zaidi na masuala ya kisiasa, kumekuwapo na mwitikio hafifu sana kwa wasomi na wasanii kutunga na kuchapisha ngonjera. Hii pengine inaweza kuwa na mawanda mapana katika kuifafanua. Kwanza, jambo hili linaweza kuwa linasababishwa na masuala ya kiuchumi kwani mtunzi yeyote yule huangalia kwanza gharama za uchapaji na masilahi yatakayopatikana kutoka katika kazi hiyo. Kutokana na kukosekana kwa soko la ngonjera inakuwa ni vigumu sana kuwalaumu wasomi kwa kushindwa kutoa machapisho mapya ya ngonjera yenye dhamira mtambuka. Miongoni mwa wataalamu wa lugha walioliona hili ni pamoja na Massamba (2003) ambaye anaeleza kuwa wasomi wengi hapa nchini hawakuvutiwa katika utunzi na uandishi wa ngonjera. Hata wasomi wachache kama vile Euphrase Kezilahabi, Penina Muhando na kadhalika waliojaribu kutunga na kuandika ngonjera waliandika kazi chache sana ikilinganishwa na sanaa nyinginezo za lugha kama vile tamthiliya, riwaya na tungo zingine za ushairi ambazo si ngonjera.

---

[6] Azimio lililowekwa na viongozi wa TANU na Afro-Shirazi mnamo tarehe 5.2.1967. Azimio hilo lilikuwa na lengo la kuondoa udhalimu, kuneemesha taifa na kuondoa aina zote za unyonyaji.

Pamoja na kukosekana kwa mwitikio wa wasomi na watunzi wengine wa kazi za fasihi, taarifa kutoka katika usaili zinathibitisha kwamba hata katika shule za msingi ambako hapo awali walimu walitumia ngonjera walizotunga wenyewe kusherehesha sikukuu na mahafali ya wanafunzi wao, kwa sasa wameacha kutumia fani hii. Kuzorota huku kunahusishwa pia na kifo cha Mathias Eugen Mnyampala ambaye ndiye alikuwa mhamasishaji mkuu wa ngonjera katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Mulokozi na Sengo (1995) wanakitaja kifo cha Mathias Mnyampala kilichotokea mwaka 1969 kama pengo kubwa katika sanaa ya ngonjera. Hii inatokana na ukweli kwamba, Mathias Mnyampala alijihusisha na shughuli mbalimbali za kukuza na kueneza ngonjera katika shule, vyuo na kambi mbalimbali za jeshi la kujenga Taifa. Vilevile, Mathias Mnyampala alianzisha vikundi mbalimbali vya utunzi na uigizaji wa ngonjera. Hivyo, kifo chake kilisababisha mambo yote hayo ambayo yalikuwa yanasaidia kukuza na kustawisha sanaa ya ngonjera kusimama. Hata hivyo, maswali kuhusu sababu na mustakabali wa ngonjera hayawezi kukomea hapo, kwani inaeleweka wazi kuwa fasihi ni hai muda wote na wala haipitwi na wakati. Hivyo, ipo haja ya kuwakumbusha waandishi wengine kuwa kifo cha Mathias Mnyampala kisiwe sababu ya kuagana na ngonjera, kwani kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi. Hivyo, ni lazima ipatikane suluhu na mbinu itakayorejesha motisha kwa watunzi na wachapishaji wa ngonjera kuendeleza aina hii ya fasihi kwa maendeleo ya taifa letu.

### 4.3 Kutokuwapo Msisitizo katika Mitaala Rasmi ya Elimu

Pamoja na ukweli kwamba ngonjera zilitumiwa sana katika ngazi za chini za elimu hasa katika shule za msingi, aina hii ya ushairi ilikosa mashiko na mwitikio kutoka katika taasisi zinazohusika na uandaaji wa mitaala ya elimu katika ngazi hizo. Wakuza mitaala wamekuwa wakijikita na kuandaa aina nyingine za kazi za fasihi kama vile tamthiliya, riwaya na ushairi wa kawaida usio na malumbano, hivyo kufanya ngonjera kuonekana kuwa ni kipera ambacho hakina umuhimu kwa jamii, jambo ambalo mwandishi anaweza kusema halina ukweli. Endapo taasisi za kielimu zingeweza kuona mapema mdororo kwenye fani hii na kuamua kulifanyia kazi jambo hili basi leo ngonjera zisingefikia hatua hii.

### 4.4 Kukosekana kwa Mwitikio wa Watunzi katika Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari ni nyenzo muhimu sana katika kuielimisha jamii. Kwa mfano, magazeti kama *Mzalendo* na *Uhuru* yamekuwa yakiandika mashairi na hadithi zilizotungwa na watu mbalimbali. Pamoja na kutoa fursa hii kwa wanafasihi, pamekuwapo na mwitikio dufu kwa waandishi kutumia fursa hii kuandika ngonjera katika magazeti haya. Hali ya kutokuthaminiwa kwa ngonjera

inadhihirika pia redioni ambapo kuna vipindi vya ushairi na vipindi vya watoto. Jambo hili limesisitizwa pia na Mgute (2012: 2) ambaye anasema:

> Ukweli usioweza kukanushika ni kuhusu kupungua kwa matumizi ya Ngonjera katika majukwaa na redioni. Jambo hili linaweza kusababishwa na mabadiliko yaliyochipuka na kurutubishwa katika mfumo wa kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimtazamo yaliyoikumba Tanzania tangu miaka ya 1990 hadi 2000.

Sababu hizi anazozitaja Mgute zilichangia kuondoka kwa umuhimu wa ngonjera kuoneshwa au kuigizwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Kwa mfano, katika vipindi vya watoto redioni, wanafunzi wamekuwa wakionesha michezo mingineyo ikiwapo uwezo wa kukariri maneno ya Kiingereza, methali, nyimbo na michezo mingineyo mingi. Hivyo, kufanya ngonjera kupoteza kabisa jukwaa bila ya kujali umuhimu wake katika kuielimisha jamii na hasa wanafunzi shuleni.

## 5.0 Mapendekezo

Katika makala hii tumejadili mambo mbalimbali yaliyosababisha ngonjera kuacha kutumika hapa nchini kama ilivyokuwa hapo awali. Kutokana na mjadala huu, makala hii inashauri njia mbalimbali zinazoweza kusaidia kuhuisha matumizi ya ngonjera kama kipera muhimu katika ushairi wa Kiswahili kama ifuatavyo: Kwanza kabisa ni kuondoa dhana potofu kuhusu ngonjera ambayo watu wengi wanaona kuwa ni nyenzo ya kuenezea siasa. Jambo la muhimu kwa sasa ni wananchi kuitumia ngonjera katika nyanja zote za maisha, hasa katika masuala ya kijamii kama vile kampeni za kisiasa, usisitizaji wa njia bora za kuhifadhi mazingira na uelimishaji wa mambo mengine mbalimbali muhimu.

Vilevile, ngonjera zitumiwe kama njia ya kufundishia masomo mashuleni kama vile uraia, kwani ni njia nyepesi kwa wanafunzi kufahamu mambo muhimu yahusuyo jamii wanazoishi. Kwa mfano, walimu wa shule za msingi wanaweza kuchagua mada ambazo zinafaa kufundishwa kwa kutumia ngonjera. Mada hizo ni zile ambazo zina sifa ya mdahalo, kama vile masuala ya haki za binadamu, jinsia, demokrasia, rushwa, uharibifu wa mazingira, kupanda kwa gharama za maisha na nyinginezo. Kwa mfano, katika *Ngonjera za UKUTA I* kuna ngonjera iitwayo "Mfungwa na Askari Jela" kama ilivyonukuliwa hapa chini:

**Askari**

Tazama wewe mfungwa, ninakuona fedhuli
Waacha ulipopangwa, wajipachika pahali
Utaniletea nongwa, kutoroka si sahali
Acha wako ufedhuli, kaba mstari kaba

**Mfungwa**

Kufungwa kwani ni nongwa, nikemewe kwa ukali?
Mfungwaji ni mpungwa, akaondoe muhali
Makosa yaliyopangwa, pengine si ya halali
Sinichunge kwa ukali, makosa kwa watu wote
(Mnyampala, 1970: 74-75).

Ngonjera hii inaweza kumfundisha mwanafunzi juu ya haki za binadamu kwani hata mfungwa anayo haki ya kujitetea anapotendewa ufedhuli. Kwa vile ngonjera zina sifa ya kimapokeo, yaani urari wa vina na mizani, itakuwa ni rahisi kwa wanafunzi kukumbuka kwa haraka mambo waliyofundishwa. Vilevile, njia hii inaweza kuwafanya wanafunzi kupenda somo na hatimaye kuja kuwa waendelezaji na watunzi wazuri wa ngonjera.

Mbali na kutumia ngonjera kama njia ya kufundishia shuleni, vyombo vya habari na asasi za serikali na zisizo za serikali zinazohusika na masuala ya lugha na sanaa vitoe hamasa kwa watu kutunga na kuandaa ngonjera. Hii itawezekana pale tu asasi hizi zikiweza kuweka mfumo rasmi hasa kwa kurekebisha mitaala ya elimu ili iwe na mwelekeo wa kuwafanya watunzi wapende kutunga ngonjera.

Jambo jingine ni kuweka kipaumbele katika ngonjera simulizi. Jambo hili linaweza kufanyika kupitia kuanzisha mashindano ya utunzi na utendaji wa ngonjera majukwaani na washindi kupata zawadi kama ilivyo katika sherehe zingine ambapo watu hushindanishwa kukimbiza kuku, kuvuta kamba, kukuna nazi, kukimbia na gunia na michezo mingineyo. Jambo hili litaamsha ari ya watu kupenda ngonjera si kwa kuangalia au kusoma tu bali pia kuendelea kufanya tafiti ili kubaini mambo ya msingi ambayo bado hayajajulikana katika ngonjera pamoja na kutoa mapendekezo ya kitaalamu kuhusu nini kifanyike ili kuipa ngonjera uhai. Pia yaandaliwe makongamano ili kujadili zaidi kuhusu ngonjera na kutumia makongamano hayo kuwaenzi wadau wakubwa walioweka misingi katika maendeleo ya ngonjera kama Mathias Mnyampala.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imejadili nafasi ya ngonjera katika fasihi ya Kiswahili. Huu ni mwendelezo wa mijadala kuhusu ngonjera nchini Tanzania. Tofauti na mijadala iliyopita, makala imeonesha sababu za kupotea kwa ngonjera na kufafanua umuhimu wake kwa jamii. Makala imemalizia kwa kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kufufua aina hii ya ushairi kwani husaidia sana katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, uelimishaji, uhifadhi wa historia ya jamii pamoja na uendelezaji wa ushairi.

## Marejeleo

Andanenga, A.S. (2002). *Bahari ya Elimu ya Ushairi*. Ndanda-Peramiho: Benedictine Publications.

Chiraghdin, S, katika Nassir, A. (1973). *Malenga wa Mvita*: *Diwani ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Nairobi: Oxford University Press.

Kawawa, R.M. (1970). Dibaji, *Ngonjera za UKUTA*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Makaka. E. (2012). Mathias Mnyampala: A Multifaceted Personality. Tasnifu ya Shahada Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Masungwa, S. (2012). Taswira na Ishara katika Ushairi wa Mathias Mnyampala. Tasnifu ya Shahada Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Massamba, D.P.B. (2003). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili, *Fasihi III: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, kur. 54-95.

Mgute, D. (2012). Mchango wa Mathias Mnyampala katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya Shahada Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. M. & Sengo, T.S.Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry (AD 1000 - 2000).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mnyampala, M. (1970). *Ngonjera za UKUTA*: Kitabu cha Kwanza. Dar es Salaam: Oxford University Press.

______ (1971). *Ngonjera za UKUTA*: Kitabu cha Pili. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ndulute, C.L. (1985). Politics in a Poetic Garb: The Literary Fortunes of Mathias Mnyampala, *Kiswahili*, 52/1 & 52/2: 143-160.

Njogu, K. & Chimerah R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.